# *NASIMAMA MLANGONI NABISHA*

. . .?. . .pia anatuokoa kutoka dhambini. Na sasa tutasoma kifungu kidogo tu, na kuzungumza nanyi dakika chache kutoka kwenye Neno la Mungu. Maana, hata hivyo, hiyo ndiyo sehemu itoshelezayo kwa yote, ni Neno. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu."

2 Sasa hebu na tuinamishe kichwa chetu kwa muda kidogo tu kabla hatujafungua Neno Lake.

3 Bwana uliye mwingi wa neema, tuna furaha asubuhi ya leo kwa ajili ya majaliwa tuliyo nayo ya kusimama katika Uwepo Wako, tukikutazamia Wewe, na kukuita Baba yetu. Tunapokumbuka katika Maandiko yetu, kwamba Wewe umesema, "Ombeni, 'Baba yetu aliye Mbinguni.'" Kujua kwamba kwa jumla sisi ni wachafu kabisa. "Tulizaliwa katika dhambi, tukaumbwa katika uovu, na tukaja ulimwenguni tukisema uwongo." Na mnyonge mwenye mashaka kama sisi, na, hata hivyo, kwa Damu ya Mwanao, Bwana Yesu, kupitia kwa neema isiyostahiliwa tuliyopewa, tuna fursa ya kutazama juu na kusema, "Baba." Loo, jinsi tunavyokushukuru kwa hili!

4 Na, leo, tungekuomba Wewe, Bwana, uichunguze mioyo yetu tunapoabudu. Tunakuja hapa si kwa kusudi lingine ila kukuabudu Wewe. Na kuona, katika siku hii kuu tunayoishi sasa, wakati, inaonekana, ya kwamba kila kitu kimeshindwa. Lakini kuna jambo moja la hakika ambalo haliwezi kushindwa kamwe, hilo ni Yesu. Kwa maana alitwambia, alipokuwa duniani, kwamba, "Mbingu na nchi zingepita, lakini Maneno Yangu hayatashindwa kamwe." Ni hakikisho la jinsi gani tulilo nalo, basi, kuweka hatima ya Milele ya nafsi zetu juu ya Neno Lake!

5 Na sasa, ni, tumepewa sisi, katika mfano wa Kitabu kiitwacho Biblia, kufahamu kwamba kiliandikwa na Roho Mtakatifu na kinaweza tu kufasiriwa na Roho Mtakatifu, jalia aje sasa juu ya Neno hili lililoandikwa, na kunena kupitia midomo ya mwanadamu, kwenye masikio ya mwanadamu, na kutoa ufahamu wa Milele. Tujalie, Baba, ili iweze kuichochea mioyo yetu, kumpenda Yeye zaidi. Na kuwa na ushirika bora zaidi Naye, kutuleta kwenye ushirika wa karibu.

6 Basi, tungekuomba, asubuhi ya leo, Bwana, kwamba kuna wagonjwa na wahitaji wengi hapa kanisani na kote nchini. Na tupate faida za kupigwa kwa mwili Wake, juu yetu leo, kwa maana imeandikwa, kwamba, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa kwake sisi tuliponywa." Na kama Daudi wa kale alivyolia, "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili Zake zote; Akusameheaye maovu yako yote; akuponyaye

magonjwa yako yote." Jalia, leo, Bwana, ya kwamba katika ibada hii, kwamba kila mtu hapa ambaye anahitaji jambo lolote, wokovu kwa ajili ya nafsi zao, au uponyaji kwa ajili ya miili yao, na tupate faida za dhabihu hii kuu zaidi leo.

7 Tunajisalimisha Kwako sasa, Bwana. Nasi tunaomba ya kwamba utanena kupitia kwetu, na utasikia kupitia kwetu, na kujibu maombi. Kwa maana tunaomba katika Jina la Mwanao mbarikiwa, Bwana Yesu Mwokozi wetu. Amina.

8 Kuna mengi mazuri sana katika Neno la Mungu, mpaka ni jambo gumu kwa mtu yeyote kuchagua Maandiko fulani. Ninaposoma Neno, nitasema, "Hili linasikika zuri sana, nitalipigia mstari. Halafu ninapoenda kwenye ibada inayofuata, nitahubiri juu ya somo *hili*." Nami nitaketi chini kwa dakika chache, nami nitamsikiliza Roho anaponena. Basi haitakuwa ila kidogo tu, mpaka nitakuwa nasoma mbele kidogo, nami nitapata kitu ambacho kinasikika bora zaidi. Nami nitalipigia hilo mstari, na kusema, "*Hili* ndilo nitakalozungumzia, nitakapoenda kanisani tena." Ndipo mu—muda si muda mnajua, Biblia yangu imewekewa alama ya mambo fulani nitakayozungumzia nitakapoenda kanisani.

9 Hivyo ndivyo Bwana alivyo mwema, na jinsi Neno Lake lilivyo la thamani kwa watakatifu Wake. Na ni majaliwa makubwa jinsi gani tuliyo nayo leo, katika saa hii, na wakati inaonekana matumaini yote yametoweka, lakini hata hivyo kupata msingi mmoja thabiti, wa uhakika, huo ni Neno.

10 Ilikuwa moyoni mwangu siku chache zilizopita, kama nilivyomwambia Ndugu Neville, ama kumtumia habari, kwa Dada yetu Wood, kwamba ningezungumza asubuhi ya leo juu ya *Yale Maandiko Ya Mkono Ukutani*. Ulikuwa ni ujumbe ambao Bwana alinipa kwenye gari-moshi, nikirudi kutoka California. Lakini katika ujumbe, ulikuwa wa kusisimua sana, na saa kama hiyo, mpaka, ikiwaacha watu. . .kupata mambo makuu, hata kwa sputniki hii ya kisasa ambayo unasikia sana habari zake, imefunuliwa katika Neno la Mungu. Na kuona saa tunayoishi, hakika tuko mwisho. Na kisha kuwaacha watu katika hali hiyo, halafu bila kuleta Ujumbe mwingine wa kuufuatisha, kutoa matumaini ya Kanisa, basi inawaacha watu kwa namna fulani wakishangaa, na kuwafanya waingiwe na wasiwasi.

11 Kwa hivyo niliwazia ningojee hadi Jumapili ijayo, nirudi, halafu ningezungumza juu ya *Yale Maandiko Ya Mkono Kwenye Ukuta,* Jumapili asubuhi. Na kisha Jumapili usiku, nizungumze juu ya, "Kanisa kunyakuliwa kabla ya ile Dhiki." Na basi kama mambo haya yamekaribia sana, basi Kunyakuliwa kumekaribia hata na zaidi, kama Kanisa linakwenda katika ile Dhi-. . .kabla ya ile Dhiki. Kwa hiyo, nina hakika mnaelewa kwamba linafanya hivyo.

12 Sasa nataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Ufunuo, katika mlango wa 3, kuhusu kanisa la siku hizi. Na kifungu cha 14, nitasoma, kuanzia. Ufunuo 3:14.

> *Na kwa malaika wa kanisa la* Laodikia *andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu.*
>
> *Nayajua matendo yako,. . .hu baridi wala hu moto: ingekuwa heri kama* ungekuwa *baridi au moto.*
>
> *Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi* wala *moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.*
>
> *Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge,. . .mwenye mashaka,. . .maskini,. . .kipofu, na uchi:*
>
> *Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto,* upate *kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi* wako *isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*
>
> *Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi: basi uwe na bidii, ukatubu.*
>
> *Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.*

13 Sasa kifungu hicho cha 20 ndipo ninapotaka kuchukua kifungu, kuona kama Mungu atatupa muktadha: *Nasimama Mlangoni Nabisha.*

14 Ujumbe huu wote asubuhi ya leo, ambao tumetoka kuusoma, ni Maneno ya Kristo Mwenyewe, baada ya kufufuka Kwake, akinena na wakati wa mwisho wa kanisa. Kama tunavyoelewa, kulikuwa na makanisa saba katika siku hiyo, makanisa saba ya Asia. Kila moja lao lilikuwa na malaika, na hao malaika walitumwa kuyaongoza makanisa haya kote katika wakati. Na sasa tunaishia kwenye wakati wa mwisho wa kanisa, Laodikia.

15 Na ni jambo lisilo la kawaida kabisa kuona jinsi jambo hili linavyoshangaza asubuhi ya leo, jinsi linavyohusika na kanisa hili la siku hizi, kuona hali za watu vuguvugu, na kutojali kanisani. Na jinsi wanavyosema ati, "Loo, tuko kwenye programu kubwa. Tunajenga kanisa la dola milioni moja. Na kanisa letu linastawi. Tuna wanachama wengi kuliko tulivyowahi kuwa nao. Mchungaji wetu analipwa vizuri zaidi. Nasi ni bora zaidi, kwa jumla." Ikiwa huo sio wito wa siku hizi!

16 Lakini, hata hivyo, Biblia ilisema, "U uchi, maskini, mnyonge, kipofu."

17 Hebu wazieni, kama mtu akiwa uchi, na maskini, na mwenye mashaka, na kipofu, wala hajui. Sasa, kama angelijua, angejaribu kujiboresha. Angekimbia kutoka mtaani akatafute nguo. Angejaribu kujiboresha. Lakini ikiwa yuko katika hali hiyo wala hajui, ni jambo la kutisha jinsi gani! Sasa, na mbele ya hayo yote. . . Hilo silo somo langu.

18 Yesu alisema, "Nasimama mlangoni, nabisha. Na mtu yeyote akifungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, naye pamoja Nami." Ni mwaliko wa jinsi gani kwa wa—watu wanaoishi katika siku hizi! Kuona vituko hivi vya kutisha ambavyo tunavitazama sasa! Pamoja na mwaliko mtukufu kama huo, "Nitasimama mlangoni na kubisha. Na mtu akisikia, na kufungua, nitaingia kwake; nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami." Ni ushirika wa jinsi gani! Ni upendeleo wa jinsi gani! Ushirika wa jinsi gani! Kusimama mlangoni, akibisha!

19 Wakati yule msanii mashuhuri. . . Siwezi kukumbuka jina lake kwa wakati huu. Alipoichora ile picha ya Yesu akibisha mlangoni. Picha yoyote, kabla ya kuwa picha maarufu, lazima ipitie kwenye ukumbi wa wakosoaji, wa—watu ambao ni wasanii maarufu wanaoikosoa hiyo picha. Wanapata kasoro zote zilizoko ndani yake. Kwa hivyo baada ya picha hii maarufu kupitishwa kwenye ukumbi wa wakosoaji, aliulizwa mtu aliyeichora. Mkosoaji akasema, "Kuna kasoro moja tu ambayo ninaweza kupata na picha yako." Akasema, "Umesahau kuweka kia kwenye mlango."

20 Ndipo mchoraji akasema, "Loo, hapana. Huelewi. Kama kia kingekuwa upande wa nje, Yeye angeinua kia na kuingia ndani. Lakini kia kiko upande wa ndani; mtu aliye ndani hana budi kuinua kia."

21 Hivyo ndivyo ilivyo. Yesu, pamoja na rehema Zake zote na huruma Zake zote, hata hivyo wewe ndiwe mtu ambaye utamruhusu aingie au kumweka nje. Una kia upande wako.

22 Mtu angegonga mlango wa mtu mwingine kwa sababu gani? Ingekuwa sababu gani? Mbona, ni kupata pa kuingilia. Anataka kuingia. Anataka, ana jambo analotaka kuzungumzia, ama jambo la kukuonyesha, mtu anapobisha mlangoni pako. [Ndugu Branham alibisha mimbarani—Mh.] Wanataka kupata pa kuingilia, ama ushirika mdogo, ama jambo la kuzungumza nawe. Hiyo ndiyo sababu Yesu anabisha mlangoni.

23 Je, ungewazia nini, kwamba kote katika nyakati, miito mingi ambayo imekuja mlangoni pa watu? Hebu turudi nyuma kwa dakika chache tu.

24 Hebu tumfikirie Kaisari Augusta mkuu katika siku za milki ya Kirumi. Vipi kama askari wa miguu angekuwa anaishi chini kwenye kibanda kidogo mahali fulani, naye Kaisari Augusta angekuja kutoka katika jumba lake la kifalme, na kushuka kwenye kibanda kidogo ambapo askari wake wa miguu aliishi,

na kubisha mlangoni? Hilo lingempa msisimko ulioje yule akari wa miguu! Mbona, mfalme mkuu wa Rumi alikuwa mlangoni pake, akijaribu kusema naye. Loo, angekuwa na furaha. Angefungua mlango na kuanguka kifudifudi, na kusema, "Mfalme mkuu, ingia katika makao yangu duni. Na chochote unachoona ambacho unataka, ni chako." Hakika, angekuwa na furaha sana kuwa na ma—majaliwa kama hayo kumkaribisha mfalme mkuu wa Kirumi katika siku zake.

25 Yangekuwa ni majaliwa yaliyoje kwa mkulima, katika siku za Adolf Hitler katika Ujerumani, Kiongozi mkuu wa Ujerumani! Kama angeshuka nyumbani kwa mtu maskini, na kubisha mlangoni, naye huyo mtu angalienda mlangoni na kuinua pazia na kutazama. Naye Kiongozi mkuu wa Ujerumani, Hitler mkuu, amesimama mlangoni pake; mtawala, dikteta wa Ujerumani. Angeweza kusema, "Vema, sistahili kwamba mtu kama huyo angebisha mlangoni pangu. Unamaanisha kwamba Hitler anataka kuzungumza na mimi, mkulima mdogo?"

26 Mbona, angefungua mlango upesi, akaanguka kifudifudi, na kusema, "Hitler, ingia nyumbani kwangu. Hakika. Chochote kilicho hapa ni chako, Kiongozi mkuu wa Ujerumani." Bila shaka, angefurahi kufanya hivyo. Si hivyo tu, bali angeheshimika kufanya hivyo, kuwazia kwamba Hitler angekuja mlangoni pake.

27 Nawe lazima uangalie umuhimu wa mtu anayebisha mlangoni pako. Hiyo ina uhusiano nalo. Kama alikuwa ni ombaomba, huenda ukawa na haki ya kufunga mlango, au kutoenda mlangoni; ikiwa hukuwa na chochote cha kumpa, na ulijisikia kuaibika mbele ya ombaomba. Lakini ikiwa alikuwa mtu muhimu . . .

28 Ningesema, leo, kama—kama Rais Dwight Eisenhower angeshuka hapa Jeffersonville, leo, na kubisha mlangoni pa mwanademokrasia yeyote mzuri, ungejisikia kuheshimiwa sana kwenda mlangoni na kumkaribisha Rais Eisenhower. Ingawa unatofautiana naye, katika siasa, bila shaka ungemthamini akibisha mlangoni pako. Kwa sababu gani? Yeye ni Rais wa Marekani. Ni mtu wa maana sana. Na ingawa unatofautiana naye, katika siasa, ingekuwa ni heshima kwa mwanademokrasia yeyote, katika mji huu au mji mwingine wowote, kumkaribisha Rais Dwight Eisenhower, kwa sababu ya umuhimu wake kama Rais wa Marekani. Yeye ni mtu mkuu, mheshimiwa, na ana cheo cha heshima.

29 Hivi majuzi tu, kutoka Uingereza, alikuja malkia. Alikwenda Kanada. Akaizuru Kanada nzima. Kisha akaja Marekani. Na kusingekuwa na mtu Merekani ila yule ambaye angefurahia kama malkia huyo angewatembelea.

30 Ungefikiria nini asubuhi ya leo, kama Malkia wa Uingereza, ingawa wewe si mmoja wa raia wake, wewe ni raia wa

Marekani, lakini, ingawa, vipi kama angekuja na kubisha mlangoni pako? Nawe ungewaona vijakazi wake, na kadhalika, wamesimama pale. Naye angesema, "Mimi ni Malkia wa Uingereza. Nimekuja kukutembelea." Hiyo ingekuwa heshima jinsi gani, kwa sababu ya umuhimu wake. Yeye ni malkia. Na mmoja wa malkia wakubwa sana duniani ni Malkia wa Uingereza. Hata hivyo, hana mamlaka katika taifa hili. Lakini kwa sababu yeye ni muhimu, ungefurahi kumkaribisha ndani. Ningefurahi kumkaribisha ndani, kujua kwamba nilipata majaliwa na heshima ya kumkaribisha Malkia wa Uingereza.

31 Lakini, loo, Yesu atasimama mlangoni na kubisha, nasi tutamweka nje. Hatutafungua mlango. Tutamwacha tu abishe. Na ni nani aliye muhimu kuliko Yesu? Niambieni ni nani aliye mkuu kuliko Yeye. Na hapa anasema, "Nasimama mlangoni, nabisha; na mtu yeyote akifungua, nitaingia."

32 Kama ungekuwa na akina Kaisari wote, akina Hitler wote, wanaume na wanawake wote wakuu duniani wamesimama mbele ya mlango wako, hungewahi kuwa na mmoja, wote wakiwekwa pamoja, hakuna kitu kingaliweza kulinganishwa na Yule anayesimama mlangoni, kila siku, na kubisha moyoni mwako: Bwana Yesu. Anataka kuingia. Anataka kuzungumza nawe. Wewe ni mmoja wa raia Wake. Uliumbwa kwa mfano Wake. Wewe ni mwanadamu ambaye umeumbwa kwa mfano wa Mungu. Naye anatamani kuzungumza nawe. Yeye kamwe haendi tu kwa wakuu, watu mashuhuri. Anakuja kwa maskini na wahitaji. "Mtu yeyote atakayeisikia Sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia na kuzungumza naye."

33 Hebu fikiria inamaanisha nini asubuhi ya leo: Kwa Mfalme wa Utukufu. Kwa MIMI NIKO aliye mkuu. Kwa ajili ya Yule aliyekuwa kwenye kichaka kilichowaka moto. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kwa ajili ya Yeye aliyeyatenganisha maji katika Bahari ya Shamu, ili wana wa Israeli wapate kuvuka. Au Yule aliyenena nalo jua likasimama kimya. Yeye aliyeumba mwezi na nyota, na akaziweka kwenye mashimo yao, ziangaze. Yeye aliyesema, "Lazaro, njoo huku," na mtu, aliyekufa, siku nne kaburini, akawa hai tena. Wazia jambo hilo! Yule aliyeingia katika tundu la simba pamoja na Danieli, na kumlinda na simba hao. Yule aliyeingia katika tanuru ya moto, pamoja na watoto wa Kiebrania, na kuupulizia moto mbali nao. Yule aliyesimama na kusema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe."

34 Anasimama mlangoni pa mwanadamu aliyeanguka, akibisha, na kujaribu kupata njia ya kuifikia nafsi. [Ndugu Branham alibisha mimbarani—Mh.] Nasi tumemkataa Mtu huyo muhimu sana.

35 Loo, unaniambia, basi, "Ndugu Branham, ninatofautiana nawe papa hapa, kwa maana tayari nimemruhusu aingie."

36 Naam, hilo ni zuri sana. Nina furaha sana kwamba ulifanya hivyo, ukamruhusu aingie. Lakini, basi, unajua nini? Inaonekana kwamba baada ya kumruhusu aingie mlangoni, una vyumba vingi vidogo—vingi vidogo moyoni mwako. Nawe utamkaribisha mlangoni, "Simama tu papa hapa, lakini usiikague nyumba yangu."

37 Unaweza kuwazia kumwambia Kiongozi mkuu kwamba angeweza kuingia, lakini hawezi kuikagua nyumba? "Sasa, Kiongozi mkuu, unaweza kusimama hapa mlangoni, Bw. Hitler, lakini usiangalie kwenye chumba *hiki*. Usiangalie *hapa*. Nina siri ndogo ambazo sitaki uzijue."

38 Hivyo ndivyo sisi, wakati mwingine, tunaojiita Wakristo, tunavyomtendea Yesu. "Unaweza kuingia ndani. Naam, ninaamini kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, lakini usiingilie biashara yangu." Mnaona? Huo ndio mstari wa hatari. Una sehemu ndogondogo moyoni mwako, milango midogo inayoingia kwenye vyumba vidogo vya siri moyoni mwako. Wakristo wanavyo. Na wengi wanaomruhusu Yesu aingie, hawako tayari kumruhusu Yesu afanye apendavyo. Kwa jumla hajakaribishwa.

39 Nikija nyumbani kwako, na unikaribishe ndani, ninajisikia kama mimi ni ndugu yako. Nami ninaweza kwenda popote ninapotaka, ikiwa kweli nimekaribishwa, nikija nyumbani kwako. Ninajisikia hivyo kama ulisema, "Karibu ndani," hiyo ina maana kwamba nimekaribishwa popote nyumbani. Ningeendelea tu. Ikiwa ninataka kulala kwa muda, nitaingia kwenye chumba cha kulala. Na ikiwa nataka ku—kula kidogo, nitaingia jikoni. Ningejisikia tu kuwa nimekaribishwa.

40 Na vipi kama ukija nyumbani kwangu, au mimi nyumbani kwako, na kusema, "Sasa, unaweza kusimama papa hapa, lakini usithubutu kufungua mlango *ule*. Usiende *hapa*"? Nisingekuwa nimekaribishwa sana.

41 Vema, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi kwa watu wanaojiita Wakristo. Unasema, "Loo, mimi ni mfuasi wa kanisa." Hilo ni sawa. Lakini mnaona, sababu ya kuwa na matatizo mengi sana kanisani, sababu ya kuwa na machafuko mengi sana kanisani, kutoridhika kwingi kanisani, si kwa sababu Yesu hayupo, ni kwa sababu kwamba Yesu hawezi kupata fursa ya kuingia mahali anapotaka kwenda. Tunavyo vyumba hivyo vidogo, nasi tunasema, "Loo, hapana, usiguse *hicho*. Sasa unaweza kuingia, lakini, loo, huo ni umbali wa kutosha. Nitajiunga na kanisa, lakini, kwa maneno mengine, hebu niendeshe shughuli zangu mwenyewe."

42 Yesu anataka kuwa mtawala mkuu wa nafsi yako. Na njia pekee anayoweza kukubariki ni pale atakapokuwa Bwana wako.

*Bwana* ni "utawala, umilikaji." Ni nani aliyekuumba? Yesu. Ni nani aliye na haki ya kila sehemu katika moyo wako? Muumba. Usiwe na siri mbele Zake. Fungua moyo wako.

43 Sasa hebu tuzungumze, kwa dakika moja ama mbili tu, juu ya baadhi ya milango hii midogo.

44 Mmoja wao ni mlango mdogo wa ubinafsi. Loo, tunauona huo sana katika moyo wa wanaokiri ni Wakristo. Ubinafsi, loo, wewe. . . mimi. . . "Ni yangu na ya kundi langu. Maadamu iko katika dhehebu langu, ni sawa. Lakini kama ni nje, kama si kanisa la Baptisti, ama si Presbiteri yangu, ama Pentekoste yangu, kama iko nje ya Assemblies, ama kadhalika, haifai kitu."

45 Basi, mnaona, Kristo hawezi kuwa na utawala. Hawezi kuwa Bwana. Ikiwa Yeye ni Bwana, Yeye ni mtawala.

46 Ukisema, "Naam, ni—ninapenda Yeye anifanyie jambo fulani, lakini kama ni. . . kama naweza kupata mengi kutoka humo. Nitaenda kanisani ikiwa itawafanya watu katika jamii yangu waniwazie mema." Lakini hutafungua mlango huu mdogo. "Nitamkubali, lakini sitamruhusu mahali *hapa* padogo, kwa sababu nimekuwa hivi tangu nilipokuwa mtoto, na ninahisi kama kidogo niko juu ya watu wa aina hiyo. Nitamruhusu Yesu aingie, lakini sitawahi kwenda kwenye mojawapo ya misheni hizo ndogo za kale, moja ya sehemu hizo ambapo wote wanapiga kelele 'Amina,' na 'Utukufu kwa Mungu,' na 'Haleluya.' Nitamruhusu aingie, lakini si—sitaenda huko." Yeye si Bwana wako.

47 "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Basi Yeye ni Bwana wako. Yeye ndiye mtawala.

48 "Nitamruhusu aingie, kama watanipeleka katika kanisa lililo bora zaidi mjini."

49 Sijali kama wangeweka. . . kama nilitaka kuingia kwenye bustani. Popote alipotaka niende, ningetaka kwenda, maadamu ananiita. Nitamruhusu aingie kwa misingi kwamba Yeye ni Bwana wangu. Chochote anachotaka kufanya, mwache afanye.

50 Kuna mlango mwingine mdogo unaoitwa kiburi. Loo, ni maskini mashetani weusi wa kutisha jinsi gani wametundikwa katika moyo huo wa kiburi, kujiona wewe ni bora kuliko mtu mwingine. "Vema, nisingewatuma watoto wangu huko. Hawavai ifaavyo. Watu wanaoenda huko hawako katika tabaka langu."

51 Ikiwa Kristo ni Bwana moyoni mwako, sisi sote ni tabaka moja kwa sababu ya Roho mmoja. Sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja. Kiburi, anahisi kidogo tu. . . Kinyongo kidogo ulicho nacho. Loo, hutaki Yesu aguse hicho, kwa sababu lingeshusha hadhi yako ya kijamii katika umma. Afadhali nishushe hadhi yangu ya kijamii katika umma, kuliko kulifuta jina langu kutoka kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-

Kondoo. Lakini hawatamruhusu aingie. Kiburi hicho kidogo kinamzuia.

52 "Ee Yesu, naam, nitajiunga na kanisa. Nitakukubali Wewe, lakini, loo, usiangalie kwenye chumba *hiki*. Kwa sababu, unaweza kuketi kwenye kiti karibu na mlango, lakini sitakuruhusu uingie kwenye chumba *hiki*." Basi hawezi kuwa Bwana wako. Hana budi kuwa na uhuru wa kuingia kwenye chumba ndani ya nyumba, kila chumba, mambo yote madogo ya siri ya maisha. Hana budi kuwa na uhuru wa kuingia kila sehemu yake, ndipo Yeye anakuwa Bwana.

53 Anataka kuja moyoni mwako kwa sababu gani? Ni kuwa Bwana wako. Anabisha mlangoni, kuwa Mwokozi wako. Na ikiwa unashikilia ubinafsi, na kiburi, na husuda, na mambo haya yote moyoni mwako, Yeye hawezi kuwa Bwana. Ingawa unakubali aingie ndani, hawezi kuwa Bwana. Anapokuwa ni Bwana, Yeye ni Bwana juu ya yote. Na hicho ndicho anachobishia. [Ndugu Branham anabisha kwenye mimbara—Mh.] "Ee, Bwana," unasema. Mruhusu aingie.

54 "Nataka kuingia na kula." *Kula* kwenyewe, ni "ushirika." Mnapofanya ushirika, mmoja na mwingine, jinsi ambavyo Bwa—Bwana pamoja nanyi ni marafiki. Nyinyi ni wenzi, na chochote mlicho nacho, Yeye anacho, pia. Chochote alicho nacho, basi, unacho, pia. Unaona, Yeye anafanyika wewe, ili upate kuwa Yeye, na kila kitu kiko katika shirika.

55 Kisha kuna mlango mwingine mdogo moyoni, ningependa kuuzungumzia asubuhi ya leo, na mlango huo mdogo ni mlango wa imani. Watu wengi wanaojiita Wakristo hawataki kuufungua mlango huo wa imani. Sasa unasema, "Bwana, unaweza kuingia. Hiyo ni kweli. Lakini siamini kwamba Biblia yote ni sahihi. Nitachukua kile ambacho kanisa langu linasema, lakini sitachukua mengine." Je, Bwana atakubariki vipi basi? Anawezaje kuwa Bwana na Mponyaji wako, ikiwa hawezi kufungua mlango wako wa imani ya moyo wako? Kama anaweza kuingia nawe utamkaribisha, atafungua mlango huo. Naye ataingia katika hiyo imani yako, Naye atakula pamoja nawe, katika mlango wa imani.

56 Loo, ninataka kumkaribisha, asubuhi ya leo, moyoni mwangu, kwenye kila chumba, kwa yote niliyo mimi. Ninataka kumkaribisha kwenye kila mlango. Niufungue wazi, na kusimama hapo na kubusu kikombe cha baraka pamoja Naye, mlangoni, na kusema, "Naam, Bwana, yote niliyo mimi, na yote niliyo nayo, na yote, ni Yako. Hebu na tusimame kwenye mlango huu, Bwana, na tufanye ushirika sisi kwa sisi. Hebu tufanye ushirika kwenye mlango wa imani, Bwana. Hebu tuwe na ushirika kwenye mlango wa kiburi, Bwana. Hebu tuwe na ushirika kwenye mlango wa ubinafsi, Bwana. Niondolee yote, Bwana." Imani!

57 Loo, unasema, “Nitajiunga na kanisa, lakini ninaamini ya kwamba siku za miujiza zimepita.” Kisha unakataa kumruhusu Bwana aingie kwenye mlango wa imani na kujidhihirisha Mwenyewe kwako. “Loo, naam,” unasema, “lakini, Ndugu Branham, mimi ni Mkristo.” Najua, mpenzi, wewe ni Mkristo, nami ninathamini hilo, kwa kumkubali Bwana, lakini unaishi chini ya majaliwa yako. Umeufunga mlango wako. Unakimbia huku na huku, na kadhalika, kwa maana huamini.

58 Ni lazima ufungue mlango huo wa imani, na umruhusu aingie, ndipo atakupa shauku ya moyo wako. “Amngojeaye Bwana atapata nguvu mpya. Watapanda juu kama tai; watapiga mbio wala hawatachoka; watatembea wala hawatazimia.” “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Loo! “Amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’” na katika kamusi asilia ya Kiyunani, inasema, “‘ukainuliwe na kutupwa baharini,’ na kuamini kwamba hilo linatendeka.” Loo, jamani! “Amini kwamba linatendeka; uliyosema yatakuwa yako.” Hakika.

59 Loo, si lazima ifanyike mara iyo hiyo. Si lazima iwe hivyo. La hasha. Mradi tu unaamini. Hapo ndipo Wakristo wanaposhindwa siku hizi.

60 Biblia ilisema, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo. Ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Kisha ungemwambia nini basi? Sasa, sio hadithi ya kubuni. Sio mawazo. Sio tumaini. Sio matamanio. “Ni hakika.” Kwa kweli ni kitu ambacho unamiliki.

61 Kwa mfano, nije kwako, na kukwambia, “Nina njaa. Lazima nipate mkate.”

Nawe useme, “Unahitaji nini? Unahitaji pesa ngapi?”

62 “Nahitaji senti ishirini na tano, kununua mkate. Nina njaa.”

63 Nawe useme, “Hizi hapa senti ishirini na tano.” Sasa, senti ishirini na tano ni uwezo wa kununua mkate. Na mradi nina senti ishirini na tano, ninao. Ni hakika. Ninaweza kuwa na furaha vivyo hivyo, nikisimama hapa na senti ishirini na tano, na mkate ukiwa kwenye Barabara ya Spring.

64 Loo, Jina Lake libarikiwe! Humruhusu aingie. Fungua mlango huo wa imani. Anaposema jambo lolote, ni Kweli. Ahadi Yake inapokuwa kwako, hiyo ni hakika. Imani inapotia nanga, kujua ya kwamba Mungu hawezi kusema uongo, limekwisha.

65 Sasa, nimepata senti ishirini na tano. Sio tu kitu nilichowazia. Ninazo senti ishirini na tano. Ninatoka nje ya mlango. Mbona, nina furaha tu sawasawa na. . .kama ningekuwa na huo mkate, kwa kuwa nina uwezo wa kununua.

66 Na kama ninayo imani, kazi zimekamilika; kama anaweza kuufungua mlango huo na kuingia, na kunipa imani ya Mungu moyoni mwangu. Imekwisha, wakati ninapoweza kumwamini

Yeye kabisa. Huenda isitokee papo hapo. Mnajua, Biblia ilisema, ya kwamba, “Musa alivumilia, akimwona Yeye asiyeonekana.”

67 Wengi wenu mmekuwa kule kuona zile Amri Kumi, ambayo imekuwa ikionyeshwa huko Louisville kwa muda. Sinema ya ajabu.

68 Sasa, “Musa alistahimili kama amwonaye Yeye asiyeonekana.” Asiyeonekana, *alivumilia*, hiyo inamaanisha, yeye “alishikilia.”

69 Ibrahimu, alipopewa ile ahadi, alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, kwamba angepata mtoto kwa Sara. Ilitosha. Saa ile ile Ibrahimu alipoufungua moyo wake, na mlango wake wa imani, na kusema, “Itafanyika.” Na alipozidi kuwa mzee, yeye. . .Biblia ilisema, “Yeye kamwe hakuwa dhaifu, katika kutokuamini; lakini alikuwa na nguvu katika imani, akimtukuza Mungu, kwa maana alijua kwamba Yeye aliweza kufanya yale aliyosema.” Hiyo hapo imani. Miaka ikapita. Sara, hakuna tofauti. “Lakini hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini; bali alikuwa hodari, akimtukuza Mungu.”

70 Sisi tunaojiita Wakristo, tunamruhusu Yesu aingie. Unasema, “Loo, mimi ni Mkristo.” Nawe unaweza kuombewa, au kupakwa mafuta, au kufanya kile ambacho Mungu anasema ufanye, au anaweza kufanya muujiza fulani mbele yako, na unaweza kuuona; na ikiwa hujaponywa mara moja, “Naam, ndivyo hivyo. Sikuupata. Nitarudi wakati ujao.” Mnaona, sio imani.

71 Inabidi umruhusu aingie, useme, “Bwana, huu hapa mlango, ingia na ushikilie.” Ndipo anapoingia mle, linatatuliwa milele.

72 “Ninasimama mlangoni nabisha.” Anajaribu kuingia kwenye mlango huo mdogo wa imani. Kama tu anaweza kupenya aingie humo, basi ni jambo lililokamilika.

73 Ninapoenda na zile senti ishirini na tano mkononi mwangu, ni sawa tu kama ule mkate, kwangu mimi, kwa kuwa nina uwezo wa kununua ki—kitu ninachotaka.

74 Nayo imani inaposhikilia moyoni, hakuna kitu kinachoweza kuitikisa. Kazi imekamilika. Mungu ameimaliza. Imekamilika milele.

75 Ninashuka mtaani. Ninavuka mto. Ninapitia kwenye kichaka cha miiba. Ninazidi kuwa na njaa, wakati wote. Sina mkate bado, lakini, wakati wote ninapoenda, nina furaha kwa sababu nina uwezo wa kununua na hakikisho kwamba mkate ni wangu.

Loo, Jina Lake takatifu na libarikiwe!

76 Wakati mimi. . .Kabla sijafika huko, ninaweza kushikwa na mkakamao; nina njaa sana. Huenda nikashikwa na mpagao, mpaka ninajikakamua sana kwenda zangu kupitia vichakani,

kama mwendawazimu. Lakini maadamu ninashikilia zile senti ishirini na tano, mkate hauna budi kuja.

77 Haya basi, mradi imani hiyo imetiwa nanga! Madaktari wanaweza kunikatia tamaa, wote, kila kitu, lakini nitakuwepo. Nitapona. Mungu alisema hivyo. Nitamruhusu aingie kwenye mlango wangu wa moyo. Imani yangu alipewa Yeye, Naye akanipa ahadi, wala hakuna kitu kitakachoizuia. Iko hapo. Imani!

78 Mlango wa imani, ni Wakristo wangapi wanaomzuia asiingie? Ni watu wangapi wa Kipentekoste wanaomzuia kuingia kwenye mlango huo wa imani? Ni Wabaptisti wangapi? Wapresbiteri wangapi? Wamethodisti? Mlango huo!

79 Loo, kuna milango mingi. Mmoja zaidi nitauzungumzia, na huo ni mlango wa macho yako. Alisema, "Wewe ni kipofu, wala hujui." Anazungumza juu ya kanisa siku hizi, kipofu kiroho.

80 Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi. Ambalo, hili siwezi kusema hadharani. Lakini kwa Ndugu Sothmann pale, na wengine wengi, Leo na Gene, na hao wengine, "Hili linaelekea wapi?" Nilisema. "Kwa nini watu hawawezi kuona mambo haya? Kwa nini hawawezi kuelewa?"

81 Hata picha hiyo inapaswa kuyatikisa mataifa, lakini ha— hata gazeti halingeweza kuandika taarifa yake. Je, George J. Lacy alisema nini, wa F.B.I.? Alisema, "Bw. Branham, hiyo itakuwa kwenye maduka ya bei rahisi, baadhi ya siku hizi, lakini si wakati ukiwa hai." Halikutoa mwangwi. Halikujibia hivi majuzi. Nilifikiria, "Kweli."

82 Wazieni juu ya yule mwendawazimu huko Portland. Wazieni juu ya wachawi huko India. Wazia juu ya yule samaki mdogo, Ndugu Wood, mtoni. Wazieni juu ya mambo yasiyoweza kukosea, uthibitisho. Na hata hivyo siwezi hata kutoka, ni vigumu, na kufanya uamsho mkubwa; nilisita. Kitu kingeachilia, lakini kinashikilia. Ni nini?

83 Hawakumjua Eliya mpaka alipoondoka. Hawakuwajua wengi wao. Hawakujua kamwe Yohana alikuwa nani mpaka alipokatwa kichwa. Hawakumjua Yesu kuwa Mwokozi wa ulimwengu hadi aliposulubiwa na kufufuka tena.

84 Mtakatifu Patrick alilichukia kanisa Katoliki, na kulipinga. Lakini baada ya kufa, walimtakatifuza kuwa mtakatifu. Hawakujua kamwe alikuwa mtakatifu mpaka alipokuwa amekufa na kuondoka.

85 Hawakujua kamwe kwamba Mtakatifu Francis wa Assisi alikuwa mtakatifu. Alilipinga kanisa katoliki. Alikuwa mhubiri anayetembea na Biblia chini ya mkono wake. Alishuka kwenda mtoni kuhubiri, nao maskini makinda wa kwenzi wakipiga mayowe. Akasema, "Akina dada wadogo, nyamazeni; ninahubiri

Neno la Mungu." Nao wakanyamaza. Lakini hawakujua hilo mpaka alipokuwa amekufa muda mrefu.

86 Joan wa Arc, ambaye aliiokoa Ufaransa, msichana huyo alikuwa mtakatifu. Alikuwa wa kiroho. Aliona maono. Alikuwa mwanamke wa kiroho. Alisikia malaika wakizungumza naye. Alisikia sauti ya Mungu. Aliona maono. Walisema nini? "Yeye ni mchawi." Nalo kanisa Katoliki likachomeka nguzo na kumtundika kwake, na kumteketeza, hao makasisi wakamchoma moto, huku akilia apate rehema.

87 Miaka mia mbili baadaye, walitambua kwamba alikuwa mtakatifu, kwa hiyo wakafanya vitubio vingi. Waliichimbua miili ya hao makasisi, waliomchoma moto, na kuitupa mtoni. Hivyo ni vitubio vingi, bila shaka. Lakini hawakumjua hadi alipokuja na kuondoka.

88 Yesu alisema, "Hawangeweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema, 'Wana macho, na hawawezi kuona; masikio, wala hawawezi kusikia.'"

89 Ni jana usiku tu, kwenye karatasi ya kwanza ya Biblia yangu, ambapo wakati fulani uliopita, katika ono ambalo Bwana alikuwa amenipa, nami nikalinena kwa kanisa. Kisha akaniambia, "Nenda Afrika, kisha urudi India."

Nikasema, "Naam, Bwana."

90 Na wakati Bw. Baxter aliponiambia, kule Canada, ama kule Chicago, kasema, "Twende India. Achana na hao Waafrika; hawatashirikiana nasi vizuri."

"Sawa," nikasema.

91 Nikalisahau. Niliporudi nyumbani, Malaika wa Bwana akakutana nami katikati ya vyumba viwili; Nguzo ya Moto, Nuru, ile ile *pale*. Naye akasema, "Wewe nenda Afrika kama nilivyosema uende."

Na mwaka mmoja baadaye, wakanishawishi tena.

92 Nami nikasahau; sikuliandika. Nami nilikuwa pamoja na mvulana wangu kule Ureno, Lisbon, Ureno. Nami nikaugua, mgonjwa, usiku kucha. Na kesho yake asubuhi, nilikuwa nikiingia kwenye beseni, kuoga kidogo. Na nikiwa njiani kuelekea kule, pale alisimama Malaika wa Bwana, akasema, "Nilidhani nilikwambia uende Afrika kwanza?"

93 Nikasema, "Bwana Mungu, sistahili kuwa mtumishi Wako." Nikasema, "Ukipenda, mchukue Roho Wako na umpe mwingine."

94 Kisha, sio tu hadi siku chache zilizopita, nilipofanya mipango ya kwenda Afrika mwaka huu, wako kule sasa hivi wakipanga. Na jana usiku, nilikuwa nikisoma katika ono, Naye Mungu alijua ya kwamba ningeshindwa hilo. Na katika hilo ono. . .Sikuwahi kuliona hadi jana usiku. Ndipo nikamwita

Ndugu Sothmann, Leo, na hao wote, karibu. Hilo ono lilisema, "Utaenda India kwanza, kisha urudi Afrika."

95 Tazama, ni—nililiandika, mimi mwenyewe. Niliandika jambo hilo, mimi mwenyewe. Nikaruka kutoka kitandani nilipokuwa nimeketi, mapema asubuhi moja, na kumwona akija humo chumbani. Nami nikaandika yale hasa aliyosema, kama a—alivyokuwa akiniambia pale. Nami nikayasoma tena, mara nyingi, nyingi, nyingi sana, wala sikuliona. Ndipo jana usiku nilipowaita hao wavulana, hilo hapo, moja kwa moja kwenye ukurasa wa kwanza wa Biblia yangu, ambapo watu wengi, wengi wamelisoma.

96 Ilisema, "Wakaja watu waliokuwa nusu uchi, na—nami nikawahubiria, nao wakafurahi. Ndipo Nuru ikamulika, baadaye, na kuwaonyesha wazungu na weusi pamoja, huko Afrika." Sikuwahi kuliona, nikilitazama moja kwa moja. Macho yetu yamefunguliwa.

97 Mungu, yafungue macho yangu, nipate kuona. Acha niangalie nyuma ya mapazia ya wakati, Bwana. Nijalie tu kuona, Bwana, kile kilicho karibu nami. Nijalie nione kile kinachokaribia kutokea.

98 Ninapowazia juu ya wanadamu waliopofushwa katika dunia hii, ambao wanaona, lakini hata hivyo hawawezi kuelewa; kumwona Mungu akija mkutanoni na kutenda mambo yale yale aliyotenda alipokuwa hapa duniani. Wanamwona Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai akifanya na kutekeleza na kufanya kama vile tu alivyofanya alipokuwa hapa duniani, na bado hawaelewi. Inawezekanaje? Kwa sababu macho yao hayajafunguliwa.

99 Yatafunguliwa, moja ya siku hizi, rafiki yangu, lakini itakuwa imechelewa sana wakati huo. Muda utakuwa umeenda. Nawe utashangaa, tena, "Unataka kuniambia, *hiki*, kwamba *Nanii* na kitu kama *hiki* kilikuwa *hivi*, wala sikujua?" Inapita juu ya vichwa vyao. Hawamshiki. Mnaelewa ninachosema? Inapita juu yao. Ni moja kwa moja . . . Nanyi mnatazamia jambo fulani kuu litukie wakati ujao, wakati ni sasa hivi, nanyi mnashindwa kuliona.

100 Mungu, ingia moyoni mwangu na ufungue milango ya macho yangu, ili nipate kuona.

101 Jinsi Kleopa na rafiki yake walivyotembea njiani siku moja, wakitoka Emau, ama wakienda Emau. Naye akienda zake kule chini, alizungumza nao, akatembea pamoja nao. Akala pamoja nao, ndipo macho yao ya ufahamu yakafumbwa. Alipoingia ndani, na wote wakanyamaza, alifanya jambo dogo walilotambua, ambalo hakuna mtu angaliweza kulifanya ila Yeye. Hiyo ni baada ya kufufuka Kwake. Na upesi, Biblia ilisema, "Macho yao yakafumbuliwa." Akafumbua macho yao, wakarudi njiani wakishangilia, na kusema, "Hakika Bwana

amefufuka, maana amekuwa nasi mchana kutwa." Macho yao yalifumbuliwa. Walikuwa na ufahamu.

102 Yesu wetu anaweza kuja moja kwa moja katikati ya watu na kufanya matendo yale yale, na nini kinatokea? Watu wataondoka na kusema, "Ni telepathia ya kiakili. Loo, huenda akawa mwanamizimu ama mpiga ramli, jambo ambalo limetukia kwa njia hiyo."

103 Loo, laiti Mungu angeyafungua macho yetu na kuturuhusu tuone mambo haya ni nini! Mlango huo wa jicho uko moyoni. Sio yale unayoona kwa jicho lako. Huko sio kuona; huko ni kuangalia. Yesu alimwambia Nikodemo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona Ufalme wa Mungu." Huuoni kwa macho yako; unauona kwa ufahamu wako. Unatazama kwa macho yako, na kuelewa kwa moyo wako. Kwa hiyo mlango wa macho yako uko moyoni wako, kwa maana ni mlango wa ufahamu.

104 "Loo, ninaelewa ya kwamba Yesu alisema angefanya hivyo katika siku za mwisho. Ninaelewa kwamba mambo haya ni ishara ya Mungu." Basi ni tofauti jinsi gani, jinsi inavyokuwa uhalisi kwako, jinsi mambo yanavyobadilika, kama macho yetu yamefumbuliwa. Yeye yuko pamoja nawe kila wakati. Anakusaidia. Anasimama mlangoni pako, kila siku, lakini hutambui.

105 Nilimsikia mhudumu mmoja akisema jambo fulani, si muda mrefu uliopita, ambalo lilinigusa. Ilikuwa kule kusini, kulikuwako na mzee huko chini, mwanamume mweusi, ambaye. . . alikuwa mzee mzuri, lakini wasingeweza kumfanya ajiweke sawa na Mungu. Yeye kamwe hangeenda kanisani, na hata hivyo alikuwa mzee mzuri. Nao wasingeweza kumfanya aende kanisani.

106 Kwa hiyo, siku moja, yeye na huyo mhudumu wakaenda kuwinda. Naye alikuwa hana shabaha kabisa. Asingeweza kupiga risasi chochote. Kwa hiyo siku hiyo, wakiwa njiani kurudi nyumbani, walikuwa wamepata mawindo mengi sana mpaka walikuwa wamelemewa na mawindo. Na jina la yule mzee mweusi lilikuwa—lilikuwa Gabrieli. Naye akamwita Gabe, kwa ufupi. Kwa hiyo alilemewa kabisa, na mawindo yakining'inia kote juu yake; angetembea kwa shida. Alikuwa anatembea nyuma ya huyo mhudumu. Baada ya muda akampiga begani, akasema, "Kasisi?"

Kasema, "Naam, Gabe, unataka nini?"

107 Kasema, "Jumapili asubuhi, nitajikuta kwenye benchi ya waombolezaji. Nitachukua nafasi yangu kanisani, hapo kuishi siku zangu zilizosalia."

108 Mchungaji huyo akasema, "Vema, Gabe. Lakini ni nini kilichosababisha hayo mabadiliko ya ghafla? Mbona, wakati tumezungumza nawe, na watu watauwa, watu watakatifu

wameomba pamoja nawe na kukushawishi, nawe ukaugeuza moyo wako?"

109 Akasema, "Bosi, unajua, najua kuwa sina shabaha. Nisingeweza kupiga chochote risasi." Kisha kasema, "Angalia mawindo niliyopata. Lazima ananipenda, la sivyo hangenipa hayo." Haya basi. Ilikuwa ni nini? Macho yake yalifunguka tu. Alitambua ni nani aliyempa hayo mawindo, mahali yalipotoka.

110 "Maksai anajua kibanda chake. Nyumbu anajua hori la bwana wake, lakini watu Wangu hawajui," alisema Bwana. Bila shaka, hawajui ambapo mambo haya mema yanatoka. Laiti macho yako yangekuwa tu yamefunguliwa, nawe ungeweza kuona.

111 Siku moja, mtu mmoja alikuwa akienda zake kando ya bahari. Alikuwa anaenda huko kupumzika. Alitaka kujiburudisha, kwa sababu alipenda. . . Alifikiri angependa kusikia shakwe wa baharini walipokuwa wakiruka juu ya maji na kushuka chini nchani mwa mawimbi makubwa meupe, huku wakinguruma na kuruka angani. Naye alitaka kunusa maji ya chumvi. Akasema, "Itakuwa ni pumziko zuri jinsi gani, kuishi kando ya ufuo wa bahari, kwa muda. Nataka kupumzika tu. Ninataka kuishi kando ya ufuo wa bahari, kuona vitu vyote inavyotoa bahari; anga za bluu, huku ikiakisi kutoka angani hadi majini. Jinsi ambavyo povu la maji ya chumvi litachemka katika mawimbi makubwa, kupiga na kufingirika!" Naye akasema, "Laiti ningeweza kusimama na kuangalia hilo, na kusikia vilio vya shakwe!"

112 Basi akienda zake ufukoni mwa bahari, alikutana na mtu akija, naye alikuwa mzee baharia, baharia kutoka baharini. Akasema, "Kwani unaenda wapi?"

113 Akasema, "Ninashuka kwenda ufukoni mwa bahari, ili kufurahia mazuri ya baharini."

114 Ndipo huyo mzee baharia akasema, "Sioni kitu cha kigeni hapo. Maji ni maji tu. Anga ni anga tu. Shakwe ni ndege mwingine tu." Unaona, alikuwa ameiona muda mrefu sana, hadi ikawa ni kitu cha kawaida kwake. Haikumsisimua.

115 Na hiyo ndiyo shida yenu watu. Mmeona wema, na miujiza, na mambo ya Kiungu ya Mungu, yakifanya na kutenda kazi, mpaka inakuwa kawaida kwako. Huyatambui tena.

116 Katika mikutano, nimeona watu, ambapo Bwana, chini ya utambuzi Wake, atazungumza moja kwa moja kwenye wasikilizaji, kama tu Yeye alivyofanya alipotembea Galilaya, na ahadi Yake tu aliyosema angeifanya. Nao watu, mara ya kwanza, wanasema, "Loo, kamwe. . . Loo, hiyo haina budi kuwa ni Bwana." Wakati mwingine, "Haina budi kuja." Na baada ya kitambo kidogo, "Vema ni kitu kingine tu." Ni kawaida. Kimepita. Hukitambui. Macho yako ya ufahamu, moyo wako, yanafungwa kwake.

117 Msisimko, baraka ya kumjua Bwana Yesu aliyefufuka amesimama katikati yetu, inapaswa kupeleka kila nafsi juu kupita kila kitu katika ulimwengu huu kingeliweza kuchangamsha. Inapaswa kukufanyia jambo fulani. Inapaswa kuitikisa imani yako mpaka ungefungua kila mlango wa imani, na kila kitu kingine, useme, "Bwana Yesu, nimiliki kikamilifu sasa. Nipeleke katika utunzaji Wako. Hapa, njoo moyoni mwangu. Ondoa ubinafsi wangu. Ondoa kutokuelewa kwangu. Ondoa mashaka yangu. Fungua macho yangu, Bwana, unijalie nione. Na unichukue mimi wote, na uwe Bwana wangu." Mpaka kanisa litakapofanya hivyo, tunatembea katika upofu. Yesu anabisha mlangoni, nasi tunamwacha nje. [Ndugu Branham alibisha mimbarani—Mh.]

Hebu na tuombe kwa muda kidogo, tunapoinamisha vichwa vyetu.

118 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa kimya, nyuso zetu zimeelekezwa kwenye mavumbi tulimotolewa. Na siku moja mwili huu upatikanao na mauti utalazimika . . . matokeo yatarudi mavumbini. Kunaweza kuwako na mtu kama huyo hapa asubuhi ya leo, ambaye hajapata kuufungua moyo wake, kwa njia hii, kwa Bwana Yesu, ambao mngemwinulia mikono yenu sasa, na kusema, "Yesu, unirehemu"? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mtu mwingine. Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo. "Ninaufungua moyo wangu wakati huu."

119 Sema, "Bwana Yesu, nichukue, wote, umilikaji kamili. Uwe Bwana wangu." Mungu akubariki, bwana. Chu- . . . "Uwe Bwana wangu." Mungu akubariki, mama. "Uwe Bwana wangu; Bwana wa fahari yangu, Bwana wa imani yangu, Bwana wa macho yangu, Bwana wa kuona kwangu, Bwana wa kusikia kwangu, Bwana wa shauku yangu." Mengi ya mambo haya ningeweza kuyazungumzia, lakini muda haungeruhusu. "Uwe Bwana juu ya yote." Mungu akubariki, mama. Ninii tu . . . Mungu akubariki, ndugu. "Nichukue, Bwana." Mungu akubariki, ndugu. "Nitwae jinsi nilivyo, Bwana." Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, huko nyuma. Hiyo ni kweli. "Nitwae jinsi tu nilivyo, na uchukue mamlaka kamili, Bwana. Usiniache nikuongoze. Wewe niongoze." Jamaa mmoja alikuwa akisema . . . Mungu akubariki, ndugu yangu.

120 Jamaa fulani alisema alitoka malishoni akamkamata farasi mdogo, hapa hivi majuzi. Akafunga kamba shingoni mwa farasi huyo mdogo, kisha akafunga nusu ya mdomo na pua kwenye uso wake, naye alikuwa akimwongoza huyo farasi kurudi kibandani. Kabla hajafika huko, huyo farasi alikuwa akimwongoza.

121 Hivyo ndivyo ilivyo. Mungu hutukamata, nasi tunajaribu kumwongoza. Mwacheni aongoze. Anajua njia. Ameipitia njia hiyo. Aliijenga hiyo barabara. Hatuijui barabara hiyo, kwa

hiyo ni kwa nini tunajaribu kuyahoji mambo haya? Hebu tujisalimishe tu Kwake, tuseme, “Bwana, niongoze. Nitafuata.”

122 Labda umekuwa Mkristo. Labda Kristo amekuja moyoni mwako, lakini hujawahi kuachilia imani yako, Kwake. Useme, “Bwana, ingia ndani. Ondoa mashaka yote moyoni mwangu. Kama Neno Lako likisema hivyo, ninaliamini. Kwa hiyo, tangu siku hii na kuendelea, ninakuchukua Wewe kama vile mimi . . . Nataka unipe yale ambayo ndugu alisema hivi punde, kama sarafu ya senti ishirini na tano kwa ajili ya mkate. Na katika maombi asubuhi ya leo, kwa ajili ya wagonjwa, nitakupokea Wewe. Ninaamini ya kwamba utafanya jambo hilo. Nami ninatembea moja kwa moja, nikishangilia, haidhuru inatukia lini. Itatukia.” Je, ungependa kufungua mlango wako wa imani, moyoni mwako, Kwake leo? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ungeufungua, basi inua mikono yako, na kusema, “Bwana, mimi hapa.” Mungu awabariki. Umati umeinua mikono yao juu.

Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Na uondoe dhambi zangu zote, (Kutokuamini
  kwangu.)
Ee niruhusu kutoka siku hii
Kuwa Wako kabisa!

123 Bwana Yesu, unaona mikono ya watu hawa. Unajua mioyo yao. Umesimama hapo. Huyo ni Wewe ukibisha. Jalia wasiangalie fumbo fulani la kisasili. Lakini jalia watazame moja kwa moja usoni mwa Mwana wa Mungu aliyesulubiwa. Na wapate ufahamu asubuhi ya leo, kuliko hapo kabla. Tujalie, Bwana.

124 Tumekuwa na magumu. Shetani ametupiga vita kwa kila njia. Hata kwa mkutano huu asubuhi ya leo, hata hapakuwapo na yeyote hapa wa kusambaziwa kadi za maombi, waweze kupangwa, kwa watu walio nje ya mji; ili uweze kuonyesha wingi wa Uwepo Wako, sawasawa na karama ya Kiungu, na mapenzi kwa nguvu Zako Mwenyewe zilizo kuu. Lakini Wewe ni Mungu anayebatilisha mambo yote. Unabatilisha magumu na hali za mambo.

125 Nami naomba, Mungu, leo, ya kwamba utaushika moyo wa kila mtu, upate njia ya kuingia kwenye kila chumba na kijisehemu. Jalia wafungue mioyo yao sasa hivi, na wale wote walioinua mikono yao, ya kuwa mbinafsi, au wa kutojali, au mambo ambayo si vile ungetaka kuwa. Inaonyesha katika maisha yao, ya kwamba Wewe huishi katika kijumba hicho. Na kifunguliwe sasa hivi. Basi, Bwana Yesu, ingia na ufanye makazi Yako kwao.

126 Na halafu, Bwana, pia tungewaombea hawa walio wagonjwa na wanaoteseka, ili saa hii, ili jambo fulani lifanyike, ambalo lingeshtua sana watu hawa kwa ufahamu wa utambuzi wa Uwepo wa Yesu Kristo, ili mioyo yao iwe wazi. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

127 Ilikuwa inatolewa, kupitia redio, na kwa mdomo, kwenye maskani, kwamba leo tungetoa kadi za maombi. Na sababu tunatoa kadi za maombi, maskanini, ni kuwachukua watu walio nje ya mji. Mnaona? Kwamba, watu walio hapa mjini, tunawaombea kila siku, ama nyakati hapa maskanini. Lakini kupata watu . . . Nguvu za upambanuzi ziko katika Kristo pekee. Na mtu yeyote anajua hilo. Hizo ziko katika Mungu pekee. Na katika . . .

128 Kristo alipokuwa duniani katika mwili wa kawaida, wa nyama, kama tunavyosimama leo hii, alitembea Galilaya na sehemu mbalimbali. Hapo alidai kuwa hana uwezo wa kuponya wagonjwa au kufanya miujiza. Alisema, "Siwezi kufanya lolote kwa nafsi Yangu. Sifanyi neno mpaka kwanza Baba anionyeshe la kufanya." Yeyote anayejua Maandiko, Yohana Mtakatifu 5, anajua ya kwamba hiyo ni kweli. Hakufanya miujiza yoyote mpaka Baba alipomwonyesha. Alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana," Mwenyewe, maskani ambayo Mungu alikaa ndani yake, mwili Wake, "Mwana hawezi kufanya neno Mwenyewe; ila lile analomwona Baba analifanya, ndilo afanyalo Mwana vile vile."

129 Na hebu angalieni alipokuja katika nchi Yake Mwenyewe, mji Wake Mwenyewe, ni nini kilifanyika? Hakuweza kufanya hivyo. Aliweka mikono Yake juu ya baadhi ya jamaa wagonjwa. Akageuka na kusema, "Amin, nawaambia, kwamba nabii, katika nchi yake mwenyewe, miongoni mwa watu wake . . . " Mnajua jinsi hilo lilivyosemwa, hilo.

130 Lakini amekuwa mwenye neema sana kwetu, kuturuhusu kuwa na mikutano michache ya aina hiyo. Hiyo ni kweli. Itafanya nini? Ni kuuacha mji huu, watu hawa, na wale walio karibu hapa, ambao hawajawahi kuwa huko nje, katika mkutano mwingine, kujua ya kuwa Yeye ni Mungu aliye hai. Alisema, "Mambo haya nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya. Mtafanya kazi zizi hizi." Akasema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona. Kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli. "Na mambo niyafanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya, hata ukamilifu wa dahari."

131 Ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho za kumalizia kipindi cha wakati wa Mataifa. Kila kitu kiko kwenye utaratibu kikamilifu, sasa hivi, kwa ajili ya wakati wa mwisho. Lakini kwenda Nyumbani kwa Kanisa, hilo ndilo Kristo anangojea. "Kama alivyokuwa katika siku za Nuhu,

mvumilivu, hataki mtu yeyote aangamie." Yeye ni kitu kile kile siku hizi. Si...Mvumilivu ndivyo alivyo sasa, hapendi yeyote apotee. Ishara na maajabu makubwa yamepita.

132 Watu wanasema, "Vema, tunatazamia enzi nzuri inayokuja." Rafiki yangu, huo wakati karibu umekwisha. Mataifa yamekwisha. Ni wakati wa mwisho. Kwa hiyo sasa ndiyo wakati wa kuwa, kumpokea Kristo na kuwa tayari. Sasa sikiliza, rafiki, sijui...

133 Sasa, hakuna kadi ya maombi humu nyumbani. Hakuna hata moja. Billy alikuwa hapa muda mfupi uliopita, ama mahali fulani. Alikuwa na takriban kadi mia moja za kusambaza, lakini watu hawakufika hapa wapate kusambaziwa. Ilibidi waanzishe ibada, ili tusiikatishe hiyo. Kwa hiyo nikasema, "Nitawaita tu watu na kuwaombea."

134 Lakini ninahisi ya kwamba Uwepo wa Kristo upo hapa. Ninajisikia kwamba nimetayarisha, na Ujumbe huu, hata, kwa ajili ya kanisa asubuhi ya leo, kwa kusudi hilo. Na kwa njia fulani adui ametuzunguka kwa njia fulani, lakini ninaamini kwamba Kristo anaweza kumbatilisha adui endapo mioyo yetu iko pamoja Naye. Na wengi wenu ninyi watu ambao mmeinua mikono yenu, bila shaka, mara tu ibada hii inapoisha, wakati wito wa madhabahuni unapotolewa, ninawatakeni mje hapa na kumshukuru Mungu kwa yale ambayo amewatendea.

Unapopokea imani, imani ni nini?

135 Tungeweza kufanyiza mstari wa maombi hapa, na kuwapitisha watu, nusu dazeni ama zaidi. Upambanuzi huo una nguvu sana, nao u—ungekuja hapa jukwaani, nanyi mngeona. Nina umri wa miaka arobaini na minane; maono yameonekana tangu nilipokuwa na umri wa miaka miwili hivi, wala hakuna hata wakati mmoja ambapo hata moja kati ya hayo limeshindwa. Hata hayo mambo, wakati ningesema, sikujua jinsi gani—jinsi inaweza kuwa kamwe. Lakini inafanya kazi hivyo tu, basi ni Mungu. Mnaona? Haina budi kuwa ni Mungu. Basi kama Mungu yupo, kulitimiza Neno Lake, kuthibitisha ya kwamba Yeye..."Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya." Ndipo anathibitisha jambo hilo kuwa ni kweli. Basi, Mungu, fungua macho yetu. Kama tungeweza kuona hilo likitimia, basi kila ahadi ni kweli.

136 Alipokuwa duniani...Ngoja kidogo. Alipokuwa duniani, alisema nini? Haya ndiyo aliyosema. Alisema, "Uharibuni Mwili huu, nitaufufua katika siku tatu." Alijuaje kufanya hivyo? Kwa sababu Daudi nabii alisema, "Sitamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitamwacha...kuiacha roho Yake kuzimuni." Alijua alikuwa Masihi aliyetiwa mafuta. Alijua hiyo ilikuwa ndiyo nafasi Yake. Na kwa kujua huo ndio ulikuwa msimamo Wake...Sasa angalieni. Akijua kwamba hiyo ilikuwa ndiyo nafasi Yake, basi aliweza kutoa tamshi hilo, kwa sababu

ahadi hiyo ilimhusu Yeye. Alisema, "Na Maandiko hayawezi kuvunjwa." Laiti ufahamu wako ungefunguka! "Maandiko hayawezi kuvunjwa." Ahadi hiyo ilimhusu, Naye alijua ilipaswa kutimia.

137 Basi sikilizeni, marafiki. Kila andiko linalokuhusu wewe, kila ahadi inayokuhusu, ni yako, kadiri hiyo ilivyokuwa Yake. Hakika, ni yako.

138 Ndiyo maana ninasimama asubuhi ya leo. Mimi, ikiwa Bwana ataniruhusu, nitamwomba afanye jambo fulani, na hapa ndani ambapo ni ngumu sana, na kadhalika. Katika ninii wangu mwenyewe . . . Si kwa sababu hamniamini mimi, bali ni kwa sababu Neno Lake lilisema jambo hili lingekuwa. Mnaona? Neno Lake lilisema itakuwa. Nitamwomba abatilishe hali ya kadi ya maombi. Mnaona? Nitamwuliza kama atafanya hivyo. Mnaona? Sininii . . .

139 Sasa kumbukeni, hebu niingie kwenye kumbukumbu, na vinasa sauti hivi vya kanda hapa vinavyoendelea, kadhaa chumbani mle. Sisemi kwamba atafanya. Mnaona? Sisemi. Nitamwomba Yeye afanye. Na kama atafanya, tutashukuru. Vipi kama Bwana . . . Ni wangapi . . .

140 Hakuna mtu huko nje aliye na kadi ya maombi. Ni wagonjwa wangapi huko nje, ambao ni wagonjwa, inueni mikono yenu, ama—ama wana . . . wanataka kitu kutoka kwa Bwana? Inueni mikono yenu, popote ulipo. Sasa naweza kuona nyuso zenu, kwa hiyo karibu ningeweza kujua wewe ni nani. Kwa hiyo, si—sininii . . . Naweza kujua . . .

141 Na kama ni yeyote wa watu wa maskanini, siwataki jamaa hao. Ninataka Bwana anionyeshe mtu fulani ambaye yuko mbali na maskani; mtu ambaye anatoka nje ya mji. Maana, kama mtu fulani kutoka maskanini . . . Ndio maana tunasambaza kadi, kuwapata watu ambao hawako maskanini. Ili kwamba . . .

142 Watu wanasema, "Naam, anamjua mtu huyo. Hivyo ndivyo upambanuzi huo unavyokuja."

143 Unakujaje Italia, Ujerumani, Uswisi, Afrika, na kote kote, ulimwenguni kote? Unafanyaje hapa na kusema mambo yatakayotokea miaka mitatu au minne, minne au mitano, na kuigonga kikamilifu kabisa? Ni Kristo.

144 Ni nani, aliyewaongoza wana wa Israeli nyikani? Kristo. Alikuwa nini wakati huo? Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Hebu wazieni hili kwa dakika moja. Alikuwa nini? Nguzo ya Moto. Nguzo ya Moto. Na alipokuja duniani, Yeye alisema ya kwamba alikuwa ni ile Nguzo ya Moto. Yeye . . .

Walisema, "Baba zetu walikula mana jangwani."

Akasema, "Mimi ndimi Mkate wa Uzima."

Kasema, "Baba zetu waliunywea ule Mwamba wa kiroho."

Akasema, "Mimi ndiye huo Mwamba."

"Mbona," wakasema, "Musa alimwona katika kichaka kilichowaka moto."

145 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Huyo "MIMI NIKO" alikuwa kichakani.

146 Alisema, "Sasa, nilitoka kwa Mungu, Nguzo ya Moto." Mungu ni Nuru, tunajua hilo. Yeye, Mungu, anakaa katika Roho, sio katika mwili. Na katika Nguzo hii ya Nuru, Yesu alisema, "Nilitoka kwa Hiyo, na ninarudi kwa Hiyo." Sasa, hiyo inaweza kuwa nje ya theolojia yako, lakini iko katika Biblia. Yesu alisema.

147 Na alipokufa, akazikwa, akafufuka tena, na wakati Mtakatifu Paulo alipokuwa akienda zake Dameski, kuwakamata wale watu, Yesu alimtokea, tena katika Nguzo hiyo ya Moto, na kumwangusha chini. Sasa, ingewezekana, mmoja angeweza kuiona na wengine wasingeweza kuiona. Hao watu waliokuwa pamoja na Paulo hawakuiona. Walisema, "Tulisikia kelele, lakini hatukuona Nuru." Lakini hiyo Nuru ilikuwa angavu sana, kwa Paulo, hata ikampofusha, naye akawa kipofu kwa siku kadhaa. Nguzo ya Moto!

148 Alikuja—Yeye alimjia Petro, gerezani, kama Nguzo ya Moto.

Naye Huyu hapa leo!

149 Na ikiwa roho ya—ya ibilisi iko ndani yako, utazifanya kazi za ibilisi. Kama wewe ni mhalifu, roho, kama roho ya John Dillinger ingekuwa ndani yako, ungebeba bunduki na kuwaua watu. Ikiwa roho ya kitu chochote ilikuwa ndani yako, itakufanya kutenda kama mtu huyo.

150 Roho wa Kristo akiwa ndani yako, atatenda kama Kristo. Atafanya kazi za Kristo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Haya basi.

Na sasa ninaweka hili kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

151 Nami naanza kuwa mzee, nami ninajua siku zangu zinaweza zisiwe ndefu sana duniani. Sijui. Hilo siwezi kusema. Natumaini nitaishi kuona Kuja kwa Bwana. Sijui kama nitakuona. Lakini, sijui kwamba nitawahi kuhubiri mahubiri mengine. Lakini mimi. . .Hatuwezi kujua hayo. Hilo liko mikononi mwa Mungu. Sijui.

152 Lakini hapa kuna jambo moja. Mimi. . .Kama tutamwomba aje katikati ya asubuhi ya leo, na atafanya jambo fulani, uthibitisho Wake usioweza kukosea, ya kwamba Yeye ni Kristo yeye yule aliyefufuka, na kufanya jambo lile lile alilofanya alipotembea ufuoni mwa pwani ya Galilaya, nashangaa ni wangapi wangesema, "Ningeacha nafasi kwenye mstari wa maombi, hata kama hakuniita. Ningepoteza nafasi yangu. Nami naamini ya kwamba moyoni mwangu ingetia nanga imani ambayo ingenishikilia imara tu kwa Kristo, na ningetoka

kwenye jengo hili asubuhi ya leo”? Kama atakuja katika miili hii ya wanadamu hapa asubuhi ya leo, na kumpa mtu fulani huko nje imani ya kutosha, kama vile yule mwanamke alivyofanya aliyegusa vazi Lake!

Naye akatazama pande zote, akasema, “Mtu fulani alinigusa Mimi.”

Nao wakasema, “Vema, kila mtu anakugusa.”

153 Kasema, “Lakini nilihisi nguvu zimenitoka.” Naye akatazama mahali pale mpaka akampata yule mwanamke, Naye akasema, akamwambia yale aliyokuwa nayo, na kilichokuwa shida yake, na kusema ya kwamba imani yake ilikuwa imemwokoa.

154 Huyo alikuwa ni Yesu. Niambie mtu yeyote aliyewahi kuishi duniani, aliyewahi kufanya jambo hilo, nje Yake. nionyeshe historia ambapo iliwahi kufanyika. Nina kitabu cha *Wafia Imani* cha Foxe. Nina *Maandishi ya Mwanzoni* cha Josephus. Nina *Nyakati za Mwanzoni* cha Pember-man. Nina *Babeli Mbili* cha Hislop. Hakujawa na jambo lolote lililotukia kama hili mpaka siku hii, hiyo ni kweli, kwa maana tuko kwenye wakati wa mwisho. Tuko kwenye wakati wa njia panda. Na Mataifa wanamalizia, si muda mrefu mpaka tutakapokuwa makaa na majivu.

155 Ninyi mpokeeni. Kama atafanya hivyo, sisemi ya kwamba atafanya, asipofanya, tutaitisha mstari wa maombi, kama atafanya hivyo, unaweza kusema, “Na ninajua mtu huyo hatufahamiani kabisa, na Mungu hufanya hivyo, nitaamini kuwa Bwana Yesu yupo, Naye atachukua kisa changu mikononi Mwake, Nitaikabidhi pale, nami nitapokea, kama zile senti ishirini na tano, nitaondoka hapa nikimshukuru Mungu kwa uponyaji wangu”? Je, mtafanya hivyo? Inueni mikono yenu, muone. Ni wangapi hapa ndani watasema utafanya hivyo? Inueni tu mikono yenu, kila mahali. Hiyo ni ajabu. Loo, jamani!

156 Sasa jiweke mwenyewe katika hali nzuri. Ufungue huo moyo. Sema, “Yesu, kama umewahi kufanya kazi moyoni mwangu, fanya hivyo sasa. Ondoa kutokuamini kwote. Ngoja niamke hapa, nijitikise. Je, ni kweli kwamba nimepitia kitu, miaka hii yote, na kukikosa? Je, nimekuwa nimefungiwa? Loo, naam, najua uko pamoja nami. Lakini je, nimekuruhusu ndani, kila mahali, kukuona?” Kama unaweza kumwona asubuhi ya leo, imani itatia nanga, na magonjwa yatatoweka. Utakuwa mzima. Amini sasa. Jamani! Natumai utaamini. Mungu, tujalie, ndilo ombi langu.

157 Sasa, kabla hatujafanya hivyo, na tuombe.

158 Ee Bwana, hii ni siku mbaya tunayoishi. Ninatambua ya kwamba kila kitu kinachoweza kutukia, itabidi kiwe ni Wewe ukiruhusu jambo hilo litendeke, Bwana. Kuna wengi hapa, dazeni moja au mbili, ambao labda wako katika hali mbaya,

mtu ambaye hatapona, ikiwa si kwa ajili Yako. Nami naomba ya kwamba utatujalia baraka hii.

159 Na, Baba, tunajua ya kwamba kuna njia moja tu ya kupokea imani. Biblia inasema, kwamba, "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Neno la Mungu linasema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Neno la Mungu linasema, "Mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya." Neno la Mungu lilisema, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Na, Bwana Mungu, tunajaribu kuingiza imani katika mioyo ya watu, kufungua milango yao, ili wapate kuona, na kujua wema wa Mungu, kuruhusu mambo haya kuwa.

160 Sasa uturehemu, Bwana. Ninapopiga magoti hapa kando ya ubao huu wa madhabahu, Ee Mungu wa rehema, utuhurumie. Ninaomba kwa ajili ya kila mtu hapa ndani, Bwana, kwa ajili ya watu wa maskanini, kwa ajili ya watu wanaotoka nje ya mji, kwa ajili ya wote. Umesema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo. Mungu atawainua. Na ikiwa wamefanya dhambi, watasamehewa."

161 Nasi tunatambua ya kwamba watu wanaopokea jambo lolote mbali na Neno, halidumu sana. Tunawawazia wana wa Israeli, jinsi wote walivyojikwaa katika mambo ya kimbinguni, kisha wakaanguka nyikani.

162 Kweli ndivyo ilivyo, Bwana, na kwa kuwa watu wana imani thabiti juu ya Neno Lako!

163 Sasa jalia, asubuhi ya leo, ya kwamba Uwepo Wako mkuu utajalia haya tunayoomba, Bwana. Ili watu wapate kujua na kuona utukufu wa Mungu. Na jalia kila mtu aliye humu ndani sasa, jalia kitu kingine, imani, ishuke kupitia mikondo ya Roho wa Mungu, na kuipaka mioyo yao mafuta sasa hivi, na macho yao yakafunguka. Kwamba, watakapoondoka kwenye jengo hili, leo, kwamba wangesema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu? Kwa maana, tuliona Utu Wake uliofufuka. Tumeshangaa, lakini sasa tunaelewa." Mungu, fungua mlango wao sasa, wa imani, na uingie ndani. Na uwafunulie, na uwajulishe njia Zako na mapenzi Yako.

164 Nisaidie, Bwana. Mimi ni maskini raia duni wa Ufalme Wako. Mimi sistahili. Na ninaomba msamaha wa dhambi zangu mwenyewe, mashaka yangu mwenyewe, na hofu, na makosa, na kutojali, na yote ambayo nimefanya. Bwana, nisamehe. Na unisaidie niwe mtumishi Wako mchangamfu, mzuri sana, nipate kulitukuza Jina Lako mbele ya ndugu zangu. Katika mambo ambayo sina nguvu ya kuyafanya, nipe nguvu, Bwana. Sio kwa utukufu wangu, hakika, Bwana, miaka hii yote umenijaribu. Ninaomba kwamba nipate neema moyoni Mwako asubuhi ya leo, ili nipate muda kidogo wa ushirika na kula pamoja Nawe. Tujalie, Bwana. Ninaomba ya kwamba utanisaidia sasa. Na

uwape watu imani, kwa maana ninasimama kutazama, nione utakalofanya. Katika Jina la Yesu. Amina.

165 Sasa, usiwe na shaka. Amini tu, kwa maana yote yanawezekana kwao waaminio.

166 Sasa, haimlazimu Bwana Yesu kufanya hivi kwa ajili yetu. Nitamwomba angalau watu watatu nisiowajua; watu watatu nisiowajua, ili Yeye anifunulie. Nini. . .Ninataka kila mmoja wenu ambaye ana haja na chochote, aombe. Na yale anayofunua, kama ni kweli, mtayajua, kama ni kweli ama si kweli. Ikiwa sio ukweli, basi sio kweli tu. Utajua wapi, wewe mwenyewe. Lakini ikiwa ni kweli, basi ukumbatie na kuupokea.

167 Angefanya nini kama angelisimama hapa asubuhi ya leo? Vipi kama Yeye alisimama hapa niliposimama, akiwa na mwili kama ninaosimama ndani yake? Kama ungesema, "Bwana Yesu, nahitaji uponyaji," unafikiri angesema nini? Angesema, "Naam, ni—nilifanya hivyo kwa ajili yako nilipokufa kwa ajili yako." Ni wangapi wanaojua huo ni ukweli? Hakika. Tayari umekamilika.

168 Basi ni nini kingekupa imani zaidi? Ili mimi na Ndugu Neville tuje tuombe, na kukuwekea mikono, kukupaka mafuta? Biblia inasema hivyo. Fanya hivyo, hilo ni jema. Tunaamini hivyo. Wakati mwingine hata hawapaki mafuta. Mara nyingine wao tu, wana upambanuzi, na kupata pepo wabaya na kuwatoa. Wakati mwingine hiyo inafanywa kwa njia hiyo. Na wakati mwingine hufanywa tu. . . Yesu alipotembea. . . Sasa kile tulicho. . .Hicho ndicho alichowapa mitume. Hivyo ndivyo mitume walivyofanya. Na mara nyingi walifanya kwa njia tofauti.

169 Sasa ni ipi ambayo ingefaa zaidi, kwa kuwa tumekuwa na mikutano mingi hapa, ni ipi ingefaa zaidi sasa? Kumwacha tu Bwana Yesu ashuke na kujithibitisha Mwenyewe ya kwamba yuko hapa, katika ulimwengu huo wa kimbinguni.

170 Je, kuna watu humu jengoni, ambao—ambao mnajua kwamba sijui una shida gani, au wewe ni nani? Inueni mikono yenu, kama wapo. Watu katika jengo, wanaojua ya kwamba siwajui, inua tu mkono wako. Naam, bwana. Nadhani ni—ni kila mahali. Vema.

171 Sasa, Bwana, ni juu Yako, Bwana. Sasa hayo ndiyo yote ninayoweza kufanya. Na, Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utalijalia, ili watu hawa waweze, katika dakika kumi zijazo, wengi wamiminike madhabahuni, huku mioyo yao ikiwa imefurika, kuona. Fungua macho yao, Bwana. Jalia. . .

172 Fungua macho yao kama wale waliokwenda Emau. Walitembea na Wewe siku nzima na hawakukujua. Lakini ulipofanya jambo ambalo walijua hakuna mtu mwingine angeweza kufanya ila Wewe, walitambua ya kwamba ilikuwa ni Wewe. Hiyo ilikuwa baada ya Wewe kufa, kuzikwa, na kufufuka tena.

173 Sasa, Baba, jalia jambo lile lile siku hii, miongoni mwa watu hawa. Na Biblia ilisema, "Watatu wangekuwa shahidi." Kwa hiyo ninaomba, Mungu, uthibitisho utafanywa asubuhi ya leo, mbele ya watu, bila kuletwa jukwaani. Yote ni katika neema Yako, na lifanyike, Bwana, naomba, kwa ajili ya Yesu, na katika Jina la Yesu. Amina.

174 Najua huu ni wakati mgumu kwenu. Vipi kuhusu mimi? Lakini kile ninachohubiri, ninaamini. Ninachohubiri, ninatekeleza; kwa neema ya Mungu, ninatekeleza. Mungu awe pamoja nami, kunisaidia, mpate kujua ya kwamba sisemi mambo haya kwa nafsi yangu mwenyewe. Macho yako yafumbuke, na useme, "Vema, nilimjua Ndugu Branham muda mrefu. Nimeona hili. Lakini ninawaambia, haidhuru yeye ni nani, anaweza kuwa mwana wa Charles Branham, ama kadhalika namna hiyo, lakini najua jambo moja, Mungu alifanya jambo fulani kupitia kwake." Basi mtazame Mungu. Usimtazame huyo mtu. Mungu hataki kunionyesha mimi; anataka kujionyesha Mwenyewe. Ni Yeye. Sasa laiti ono litakuja!

175 Hili hapa. Dada Snyder. . . Ni—ninajaribu kuangalia mbali na jambo hilo, unaona. Na, Mungu, uturehemu.

176 Huyu hapa mtu ameketi papa hapa. Ono liko juu yake, akinitazama moja kwa moja. Nadhani mimi ni mgeni kwako. Unajaribu kuachana na tabia, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Ninajaribu kuachana na tabia hiyo, bwana."—Mh.] Kuachana na uvutaji wa sigara, ndio unaojaribu kuacha. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Hapana, ninamaanisha huyo kijana mwanamume anayeketi nyuma *hapa*. Sikujui. Sisi hatufahamiani, hiyo ni kweli, mmoja kwa mwingine? Kama ndivyo, punga mkono wako *hivi*. Je, ndivyo hasa ulivyokuwa ukiomba wakati huo? Vema.

177 Unaamini? Ni kitu gani kinachofanya hivyo? Aligusa nini? Biblia ilisema, kwamba, "Yeye ndiye Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Kamwe hakunigusa mimi. Sijawahi kumwona mtu huyo. Lakini alimgusa Kristo, ambaye yuko hapa, naye Kristo alitumia midomo na macho yangu, kunena.

178 Umeinua mikono yako, kijana. Naona unaendelea kuishika mikono yako. Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Je, utakubali nilichokwambia? Ikiwa ungekuwa na imani na kuamini! Unafikiri angeokoka kweli? Msichana rafiki yako, unamwombea, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] U-huh. Unataka aponywe, pia, sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Wewe! Hiyo ni kweli, sivyo? ["Naam, bwana."] Sasa mwamini Mungu, nawe utalipokea. Hatufahamiani, kijana. Sijawahi kukuona. Hivi hatufahamiani? Inua mikono yako yote miwili, juu, kama hatufahamiani.

Sijawahi kukuona maishani mwangu; hujawahi kuniona. Sasa nani . . . Waweza kuketi sasa, na kupokea kile ulichoomba. Imani yako imekupa wewe.

Mnaamini?

179 Ilikuwa ni mzaha muda mfupi uliopita, sivyo, dada? Lakini sio mzaha sasa. Nilijua Bwana angefanya hivyo, ama nilifikiri angefanya. Mungu hawezi kuchezewa. Yeye ni halisi. Kama unaweza kuamini!

180 Hapa kuna mwanamke ameketi nyuma namna hii. Anaomba kwa ajili ya mtu mwingine. Huyo mwanamke ana fadhaa. Yeye ni Mkatoliki, kwa imani. Hiyo ni kweli. Anaishi kwenye Barabara ya Meigs, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Vema. Unaamini? Basi pokea unachoomba, ikiwa unaweza kuamini.

181 Vipi kuhusu wewe huko nyuma? Mtu fulani apate ninii . . . Hu—huko nyuma sana. Kristo anajua hasa mahali unapoketi. Ninakupa changamoto, katika Jina la Yesu, kuamini sasa. Yuko hapa. Roho Wake yuko hapa. Nguvu Zake ziko hapa.

182 Hapa ameketi mwanamume anayeketi kule nyuma kabisa, ananitazama sasa. Amevaa tai ya kijani, suti ya kijivu, kitu kama hicho. Anaomba pia. Anataka kuponywa aina fulani ya ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa tumbo tumboni na matumbo. Hiyo ni kweli. Wewe unayeketi hapo nyuma. Hebu nikwambie wewe ni nani. Ulikuwa kwa daktari jana, naye akakuchunguza. Hiyo ni kweli. Sikujui, unajua hilo, lakini Mungu anakujua. Imani yako ilikuokoa, bwana. Mungu aliye hai asifiwe!

183 Huyo mama aliyeketi moja kwa moja nyuma yake, katika safu inayofuata, kama tatu, huko nyuma. Hapo, ukimwombea mama mkwe wako, hali ya ulemavu. Kama utaamini, sawa.

184 Kuna jamaa mdogo ameketi pale, ameinua mkono hadi kinywani, akinitazama, nyuma kabisa kuelekea nyuma. Ameweka mkono wake kinywani mwake. Anaomba. Kuna roho ya huzuni inayomzunguka. Anapangusa macho yake. Naweza tu kuona, kijana. Anamwombea mtu fulani. Huyo ni jamaa yake. Mwanaume huyo amekuwa kwenye hospitali ya vichaa. Ni jamaa mdogo. Ni shemeji, ugonjwa wa fadhaa, ugonjwa wa kiakili. Hiyo ni kweli, bwana. Kuwa na imani, na Mungu atakushindania.

185 Ninatoa changamoto kwa imani yenu katika Kristo. Je, mnamwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hao ni watatu? Loo, ni . . . Hao ni zaidi ya hiyo, sivyo? Sasa mnaamini? ["Amina."] Imani yako imetulia? Moyo wako umefunguka? Inua mikono yako, ikiwa moyo wako umefunguka. Je, mlango uko wazi? ["Amina."]

Basi hebu tuinamishe vichwa vyetu.

186 Bwana, njoo karibu sasa, Yesu mbarikiwa. Ee Mungu, ninakushukuru Wewe, Baba, kwamba ulitujalia baraka hizi. Ili wao, watu waliopo sasa, watajua ya kwamba haikuwa ni mtumishi Wako. Ilikuwa ni Mungu wa Mbinguni, ambaye ametuheshimu asubuhi ya leo kwa kuja katikati yetu, na kuruhusu jambo kama hilo lifanyike. Kukithibitishia kizazi hiki cha Mataifa, kabla hakijafutiliwa mbali kutoka duniani, ya kwamba Wewe ndiwe Masihi. Wewe ni Bwana Mungu wa Mbinguni. Uko hapa, Ee Bwana.

187 Tafadhali, nakuomba utoe mshtuko mmoja zaidi kwa watu hawa, tuseme, au kufungua ufahamu wao, kwa maana wataendelea katika dhambi zao kama wasipokuamini na kukiri mashaka na kutokuamini kwao. Na ije baraka kwa watu, sasa hivi, hata watajua ya kwamba Roho Mtakatifu yupo, na kwamba yuko tayari kuwaponya, kama vile alivyo tayari kumponya mtu yeyote. Imewekwa msingi juu ya, "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Bwana, tujalie. Pia jalia nguvu Zako za uponyaji ziingie ndani ya mioyo ya watu, sasa hivi, na kumponya kila mmoja wao. Ninakushukuru, Bwana.

188 Shetani anapoingia kama simba angurumaye, Roho wa Bwana huinua beramu juu yake, na kumwangusha, Shetani mkuu anayedai kuwa ndiye Mkuu. Lakini Bwana wetu Yesu ndiye Mkuu, Yeye na Baba Mungu.

189 Nami naomba, Bwana, ya kwamba sasa hivi, kwa Roho Wako, ya kwamba utapita katikati ya wasikilizaji na kumponya kila mtu. Kupitia Jina la Bwana Yesu tunaomba. Amina.

190 Unaamini kuwa umeponywa? Unaamini jambo hilo, kwa kupigwa Kwake? Je, kuna kitu kimetia nanga ndani ya moyo wako? Je, una zile senti ishirini na tano ambazo zitakufanya utembee kutoka humu jengoni? Unazo? Inua mkono wako. "Ninazo. Ni imani iliyotiwa nanga. Sijali inachukua muda gani, siku ngapi, saa ngapi. Nina uwezo wa kununua wa uponyaji wangu sasa hivi, na nitatembea kutoka kwenye jengo hili, sasa hivi, sawa tu na kama kwamba nilikuwa mzima kabisa." Unaweza kuwa, unaposimama kwa miguu yako. Huenda usiwe; unaweza usiwe, kwa majuma kadhaa. Sijui. Lakini utakuwa, kama una imani ya kuamini jambo hilo. Mungu ni imani. Mwamini kwa moyo wako wote.

191 Sasa jifungie tu ndani pamoja na Mungu, sasa. Sasa anza tu hivi, "Bwana, naamini. Bwana, naamini. Mashaka yangu yote yamezikwa kwenye Chemchemi. Bwana, naamini. Mwokozi, inua imani yangu Kwako, hata inaweza kuuhamisha mlima. Ee Bwana, unaweza kuwa umekosea? Huwezi kukosea. Kwanza, kama Ndugu Branham hakuwa na neno moja la kusema, Neno Lako lilisema hivyo. Ndipo, kwa neema, ulimruhusu Ndugu Branham kutazama juu ya jengo hili kwa watu wengi, kufanya jambo lile lile ulilofanya ulipotembea Galilaya. Kama nimekuwa

na shaka moyoni mwangu, Bwana, basi iondoe, kabla siku zangu hazijaisha. Kabla sijaitwa, kujibu kwenye Hukumu, niondolee dhambi yangu ya kutokuamini. Na unifanye kuwa Wako sasa hivi. Jalia niwe Wako." Mungu awabariki, ndiyo maombi yangu. Na wale . . .

192 Sasa wakati mkiomba, mkiwa mmejifungia ndani pamoja na Mungu, kulikuwa na wale walioinua mikono yao, ambao walitaka kutembea pamoja na Mungu, mlitaka kumfungulia mioyo yenu. Madhabahu iko wazi sasa, rafiki yangu. Ningewaalika kila mmoja wenu kuja hapa madhabahuni na kupiga magoti, na kusema, "Bwana Yesu, uturehemu. Nataka Uingie moyoni mwangu. Ondoa mashaka yangu yote. Ondoa hofu zangu zote. Ondoa ubinafsi wangu. Toa kila kitu, Nawe uingie ndani. Ingia moyoni mwangu na uwe Bwana. Loo, ninaamini Wewe ni Mwokozi wangu, lakini hujawa Bwana wangu."

193 Mungu akubariki, ndugu. Jina la mtu huyu ni Davis. Anatoka Virginia. Yuko hapa kuacha tabia ya kuvuta sigara, na kinyongo kidogo ambacho ameshikilia moyoni mwake dhidi ya mpendwa fulani tangu alipokuwa mtoto. Hiyo ndiyo sababu yuko madhabahuni, asubuhi ya leo.

194 Sasa njoo. Unaalikwa kuja madhabahuni sasa. Piga magoti hapa mbele ya Kristo wa Mungu. Usiangalie maskani ndogo nyenyekevu. Angalia ni Nani aliye humu ndani, asubuhi ya leo, Mwokozi wetu aliyebarikiwa. Waweza kuja? Umealikwa. Bwana Yesu anakungojea uje, ili kila roho (utakaso) itoke moyoni mwako.

. . . watoto Wake wapendwa.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia motoni, lakini wote kupitia kwenye Damu;
Wengine kupitia huzuni kubwa, lakini Mungu anatoa wimbo,

Panda juu, asubuhi ya leo, piga magoti katika Uwepo Wake.

Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa;
Wakati mwingine katika bonde katika giza la usiku,
Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwenye Damu;
Wengine kupitia huzuni kubwa, lakini Mungu anatoa wimbo,
Katika msimu wa usiku na mchana kutwa.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwenye Damu;
Wengine kupitia kwenye huzuni kubwa, lakini Mungu anatoa wimbo,
Katika msimu wa usiku na mchana kutwa.

Ingawa huzuni inatupata, na Shetani anapinga,
Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa;
Kupitia neema tunaweza kushinda . . .?. . .
Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa.

Je, hutamruhusu akuongoze?

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia motoni, lakini wote kupitia kwenye Damu;
Wengine kupitia huzuni kubwa, lakini Mungu anatoa wimbo,
Katika msimu wa usiku na mchana kutwa.

195 Sasa umealikwa, tunapoimba; ikiwa Mungu anabisha moyoni mwako, upate kufungua moyo wako, kuona Uwepo Wake, kufurahia baraka za Yeye kuwa Bwana wako, mtawala wako. Je, hutasahau tu ya kwamba uko katika maskani hii ndogo ya kale? Na uje hapa kwenye Kiti cha Enzi cha neema Yake, na kupiga magoti pamoja na watu hawa wengine wanaolia, na kuufungua moyo wako, ili aweze kufungua ufahamu wako, ili uwe mtoto Wake na kumtumikia. Kwa mara nyingine tena tunaimba, mstari wa mwisho wa wimbo huu. Umealikwa. Sasa njoo.

Mbali na matope, na mbali na udongo,
Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa;
Huko juu katika utukufu, siku ya Milele,
Mungu huwaongoza watoto Wake wapendwa.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwenye Damu;
. . . lakini Mungu anatoa wimbo,
Katika msimu wa usiku na mchana kutwa.

Kwa upole.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia kwenye mafuriko,
Wengine kupitia kwa moto, lakini wote kupitia kwa Damu;
Wengine kupitia huzuni kubwa . . . (Huelewi?) . . . wimbo,

Katika msimu wa usiku na mchana kutwa.

196 Kwa uchaji, tunainamisha vichwa vyetu sasa katika Uwepo wa Mfalme mkuu wa utukufu, Mfalme mkuu wa amani. Jinsi tunavyoshukuru jinsi mmeinua mioyo yenu wazi kwa Roho huyu mkuu aliyepo sasa. "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Haijalishi mahitaji yako ni nini. "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Mungu hufanya hivi kwa ajili yetu.

197 Sasa, watoto, mkiwa humu jengoni, popote pale, inamisheni tu vichwa vyenu. Iweni na kicho kabisa wakati ndugu yetu anapoomba, nawe utapokea hicho ulichoomba. Bwana awabariki sana sasa, wakati dada akiendelea na kuimba kwake, polepole sasa. [Ndugu Neville anaomba—Mh.]

57-1208 Nasimama Mlangoni Nabisha
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org